## MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI MACHI, 2026 NA MWELEKEO KWA MWEZI APRILI, 2026.

### Dondoo za tathmini ya Machi, 2026 na mwelekeo wa Aprili, 2026:

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Machi, 2026 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa kwa mwezi Aprili, 2026 nchini.

i. Katika kipindi cha mwezi Machi, 2026, maeneo mengi ya nchi yalipata vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo, pamoja na vipindi vya mvua kubwa katika baadhi ya maeneo. Hali hii ilisababisha athari ikiwemo mafuriko, kutuama kwa maji na uharibifu wa mali na miundombinu.

ii. Katika kipindi cha mwezi Aprili 2026, mvua zinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi nchini. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

iii. Hali ya joto la kawaida inatarajiwa kujitokeza katika maeneo mengi katika kipindi cha mwezi Aprili, 2026.

### 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI MACHI, 2026.

Katika kipindi cha mwezi Machi, 2026 vipindi vya mvua zilizoamabatana na ngurumo vilijitokeza katika maeneo mengi ya nchi. Kuimarika kwa Ukanda mvua (ITCZ) pamoja na wimbianga (MJO) kulichangia uwepo wa vipindi vya mvua kubwa zilizoambatana na ngurumo pamoja na upepo mkali kwa baadhi ya nyakati. Hali hii iliweza kusababisha mafuriko, kutuama kwa maji, kuathiri shughuli za kiuchumi, uharibifu wa miundombinu na mali pamoja na vifo.


Kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 144.9 kilipimwa katika kituo cha hali ya hewa Kilwa (mkoa wa Lindi) mnamo tarehe 22 Machi, ikifuatiwa na milimita 126.4 katika kituo cha Zanzibar na milimita 117.0 katika kituo cha Moshi (mkoa wa Kilimanjaro) mnamo tarehe 25 na 1 Machi, 2026 mtawalia. Vituo vilivyopima mvua milimita 60 au zaidi ni kama inavyoonekana katika kielelezo Namba 1.

Kwa upande mwingine, hali ya joto la wastani hadi joto kali ilijitokeza katika baadhi ya maeneo, hususan mwambao wa pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki. Kiwango cha juu zaidi cha nyuzi joto 35.2 °C kiliripotiwa katika kituo cha Mlingano (mkoa wa Tanga) mnamo tarehe 19 Machi ikifuatiwa na nyuzi joto 34.2 °C katika kituo cha Zanzibar mnamo tarehe 2 Machi 2026.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu “N”, Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*727B - 03/2026*




Kielelezo 1: Vituo vilivyopima viwango vya mvua milimita 60 au zaidi katika mwezi Machi, 2026

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI APRILI, 2026

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Joto la Bahari katika eneo la tropiki ya kati ya Bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuendelea kuwa la wastani hadi juu kidogo ya wastani ikiashiria kuendelea kwa hali ya kawaida ya ENSO katika kipindi cha mwezi Aprili, 2026. Joto la bahari katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi, karibu na Pwani ya Afrika mashariki, linatarajiwa kuwa la wastani hadi juu kidogo ya wastani, wakati eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa na joto la bahari la wastani. Hali hii inatarajiwa kuongeza upepo wenye unyevu kuvuma kuelekea ukanda wa pwani ya nchi yetu na mikoa ya jirani. Joto la bahari katika eneo la kusini mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) linatarajiwa kuwa la chini kidogo ya wastani. Hali hii inatarajiwa kuchangia kusababisha upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka misitu ya Congo kuelekea maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi yetu. Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa Afrika inatarajiwa kuimarika kidogo na kupelekea Ukanda mvua (ITCZ) kusogea kuelekea kaskazini.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu “N”, Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

## 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI APRILI, 2026

Katika kipindi cha mwezi Aprili, 2026 mvua zinatarajiwa kuendelea katika maeneo nchini, huku kukiwa na upungufu kidogo ukilinganisha na mvua za mwezi Machi, 2026. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo nchini na kusababisha mafuriko katika baadhi ya maeneo. Kuelekea mwishoni mwa mwezi mvua za Msimu zinatarajiwa kuisha katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka.
Hali ya joto kwa ujumla inatarajiwa kuwa ya wastani katika maeneo mengi. Aidha hali ya joto hadi joto kali inatarajiwa kuendelea katika maeneo machache yanayotarajiwa kuwa na upungufu wa mvua. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika maeneo machache katika wiki ya pili ya mwezi.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika wiki ya pili ya mwezi.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya pili ya mwezi.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya pili ya mwezi.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika maeneo machache katika wiki ya pili ya mwezi, ikifuatiwa na upungufu kuelekea mwishoni mwa mwezi.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Mvua zinayoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa kati ya wiki ya kwanza na ya pili katika maeneo machache, ikifuatiwa na upungufu katika wiki ya tatu na ya nne.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi, ikifuatiwa na upungufu kuelekea mwishoni mwa mwezi.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Vipindi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa kwa wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi, ikifuatiwa na upungufu kuelekea mwishoni mwa mwezi.

## 2.3 MATARAJIO KWA MWEZI MEI, 2026

Katika kipindi cha mwezi Mei, 2026 mvua zinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo nchini. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

## 2.4 USHAURI

Mvua zinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi nchini. Aidha, vipindi vya mvua kubwa vinatarajiwa kujitokeza, hivyo wananchi wanaoishi katika maeneo yanayoathiriwa na mafuriko wanashauriwa kuendelea kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari zitakazojitokeza.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Aprili, 2026 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz